

**MABADILIKO YA SHULE/TAHASUSI KWA WANAFUNZI
WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO NA
VYUO VYA UFUNDI MWAKA 2015**

Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) ilitangaza majina ya wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuvo vya Ufundi mwaka 2015, **tarehe 30 Juni, 2015**. Baada ya majina haya kutangazwa, OWM-TAMISEMI imepokea maombi mengi toka kwa Wazazi/Walezi na Wanafunzi ya kuomba kubadilishiwa Shule na/au Tahasusi kutokana na sababu mbalimbali. OWM-TAMISEMI imeyachambua maombi haya kwa kuzingatia sababu zilizotolewa na waombaji, uwepo wa nafasi kwenye shule walizomba na ufaulu wa mwanafunzi aliyeomba kubadilisha tahasusi.

Kwa wanafunzi ambao majina yao **hayajaonekana kwenye orodha hii na wale waliobadilishiwa shule/tahasusi** mnahimizwa kwenda kuripoti kwenye shule mlizopangiwa na ikumbukwe kuwa tarehe ya mwisho ya kuripoti ni tarehe **31 Julai, 2015**. Kushindwa kufanya hivyo, nafasi zao zitagawiwa kwa wanafunzi waliokosa nafasi.

Imetolewa na

KATIBU MKUU OWM-TAMISEMI